

KINONDONI YATOA MAFUNZO YA KUKUZA MITAJI MIDOGO KWA WAJASIRIAMALI.

Katika kutekeleza kwa vitendo na kwa ufanisi wa kiwango cha juu sera ya kuwawezesha wanawake,vijana na walemavu , kujikwamua na kuondokana na umaskini, Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imetoa mafunzo kwa wafanyabiashara ndogondogo yanayolenga kukuza mitaji yao na kujiimarisha kibiashara na kiuchumi.

Mafunzo hayo yalikuwa katika awamu mbili ambapo katika awamu ya kwanza ilihusisha viongozi yaani wenyeviti na makatibu wote wa Masoko ya Manispaa, na katika awamu ya pili ilihusisha wafanyabiashara wadogo zaidi ya elfu kumi.

Mratibu wa Mafunzo hayo ambaye pia ni mkuu wa Idara ya maendeleo ya jamii na ustawi wa jamii Bi.Halima kahema amesema kuwa lengo la mafunzo hayo ni kuwawezesha wafanyabiashara ndogondogo kufanya biashara zao kwa ufanisi, kukuza mitaji yao kwa kujiunga katika vikundi na hata kuunda vyama vya ushirika SACCOS.

Kwa mujibu wa mratibu huyo amesema kwa kutambua changamoto iliyopo ya mitaji midogo kwa wafanyabiashara wadogo kuwa ni tatizo, hivyo wamechukua jukumu la kuwafundisha namna ya kukuza mitaji yao kwa kusaidiana na kushirikiana pamoja kwani kwa kufanya hivyo wanaweza wao wenyewe kupunguza tatizo hilo la mitaji midogo.

Aidha mafunzo hayo pia yamelenga katika kuwaelimisha namna na umuhimu wa kutumia vyombo vya fedha (**Benki za Biashara**) kupata mikopo yenye riba nafuu itakayowazesha kujikwamua kiuchumi na kuondokana na umaskini.

Bi. Kahema anasema kuwa mafunzo hayo yamelenga pia kuelezea umuhimu wa kurasimisha biashara kwa maana ya kuzisajiri na kufanya biashara kwa mujibu wa sheria ,taratibu na kanuni.

Zaidi ya wafanyabiasha elfu kumi wamepata mafunzo hayo na kunufaika nayo.



Mstahiki Meya Manispaa ya Kinondoni Mh Benjamin Sitta akikabidhi hundi ya shilingi milioni 10 kwa wajasiriamali.